Jarida la

Ligi Kuu

Oktoba 2026



Simba Yafuta ‘Uteja’ ‘Kariakoo Dabi’

www.ligikuu.co.tz



Yaliyomo

- Neno la Afisa Mtendaji Mkuu..... 2
- Simba Yafuta Uteja 'Kariakoo Dabi'...'..... 4
- Teknolojia iliyoleta Mageuzi ya Soka Tanzania 6
- TPLB Yaingiza Teknolojia mpya Ligi Kuu ya NBC 8
- Simba yatawala Msimamo Ligi Kuu ya NBC 10
- Siri nyuma ya 'Unbeaten' Simba, Azam na Dodoma Jiji 13
- Ligi Kuu ya NBC na Rekodi mfululizo mashindano ya Kimataifa 14
- NBC Championship Ngoma inogile.....16
- Boli na Fasheni.....17
- Pazia la First League Lafunguliwa.....20







MAELEZO YA UCHAPAJI

Jarida hili huchapishwa kila mwezi na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania - TPLB

Mhariri Mkuu
Cornel Barnabas

Mhariri Habari
Yahaya Abushehe

Mhariri Msaidizi
Honest Mwanitega

Mpiga Picha
Loveness Bernard

Msanifu Kurasa
James Onesmo

Wachangiaji
Salma Seif
Pancras Remidius
Cynthia Michael
Sakina Abdoul
Collins Mwesigwa



Bodi ya Ligi Tuu Tanzania

Ghorofa na 14, NSSF Mafao House,
Barabara ya Uhuru - Ilala,
Dar es Salaam
S. L. P 79041 Dar es Salaam

www.ligikuu.co.tz
info@ligikuu.co.tz

Ligi Kuu

ligikuu | championshiptz | firstleague

tplboard

ligikuu

Ligikuu

LIGI KUU TV

NENO LA AFISA MTENDAJI MKUU



Karibu katika toleo la mwezi Oktoba 2026 la Jarida la Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), linaloendelea kuwa jukwaa muhimu la kuhabarisha, kuelimisha na kuonesha maendeleo ya soka la Tanzania.

Mwezi Oktoba umekuwa na matukio muhimu yanayoonesha kukua kwa thamani, ushindani na mvuto wa Ligi Kuu ya NBC. Moja ya matukio yaliyoipa soka letu heshima kubwa ni mafanikio ya klabu nne za Tanzania kufuzu hatua ya makundi ya mashindano ya klabu barani Afrika kwa msimu wa pili mfululizo. Mafanikio haya ni kielelezo cha ushindani unaozidi kuimarika ndani ya ligi yetu na nafasi inayozidi kujengwa na soka la Tanzania katika ramani ya Afrika.

Aidha, Dabi ya Kariakoo kati ya Simba SC na Young Africans SC imeendelea kuthibitisha ukubwa wa soka la Tanzania. Mchezo huo haukuwa tukio la ushindani wa kimichezo pekee, bali pia jukwaa la kuitangaza Tanzania kupitia soka, ambapo ulivutia zaidi ya waandishi wa habari 180, wakiwemo waandishi 16 kutoka nje ya nchi. Haya ni mafanikio yanayoonesha namna ambavyo matukio ya ligi yetu yanavyoweza kuwa bidhaa yenye mvuto wa kitaifa na kimataifa.

Katika kuendelea kuboresha usimamizi na ubora wa mashindano, Bodi inaendelea kuweka mkazo katika matumizi ya teknolojia, usalama wa wadau na ufanisi wa shughuli za uendeshaji wa ligi. Maboresho ya mifumo ya kidijitali, matumizi ya mfumo wa Football Video Support (FVS), pamoja na matumizi ya vifaa vya kupima ubora wa hewa katika vyumba vya kubadilishia nguo ni sehemu ya dhamira yetu ya kuhakikisha mazingira ya ushindani yanakuwa salama, ya kisasa na yenye kuzingatia viwango vinavyotakiwa.

Sambamba na hayo, tunaendelea kuimarisha mifumo ya kibiashara na kiutawala ili kuongeza thamani ya Ligi Kuu ya NBC, kuvutia uwekezaji na kujenga mazingira bora kwa klabu, wachezaji, wadhamini, wabia wa kibiashara na wadau wengine wa soka.

Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wadhamini wetu, washirika wa kibiashara, klabu, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), vyombo vya habari na mashabiki kwa mchango wao katika maendeleo ya ligi. Mafanikio tunayoyapata ni matokeo ya ushirikiano na dhamira ya pamoja ya kuendeleza soka letu.

Bodi ya Ligi Kuu Tanzania itaendelea kujikita katika ubunifu, uwajibikaji, matumizi ya teknolojia na usimamizi wenye viwango, tukilenga kuifanya Ligi Kuu ya NBC kuwa miongoni mwa ligi zenye ushindani, thamani na mvuto mkubwa barani Afrika

Cornel Barnabas

Afisa Mtendaji Mkuu
Bodi ya Ligi Kuu Tanzania

Simba Yafuta ‘Uteja’ ‘Kariakoo Dabi’

Oktoba 10, 2026 katika uwanja wa Uhuru Dar es Salaam ilichezwa ‘Dabi’ ya Kariakoo ambapo timu ya Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya watani wao wa jadi Young Africans katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC

Ushindi huo uliifanya Simba kupata heshima kubwa mbele ya mashabiki wake na kuvunja ukimya wa kukosa ushindi dhidi ya Yanga katika michezo ya Ligi Kuu ya NBC uliodumu kwa zaidi ya miaka mitatu.

Upekee wa mchezo huo ulikuwa kwa timu zote kuongozwa na makocha kutoka nchi ya Afrika ya Kusini ambapo Steven Barker alikuwa mwenyeji wa Kocha Manqoba Mngqithi wa Young Africans ikiwa ni mara ya kwanza kukutana ndani ya Ligi Kuu ya NBC licha ya kukutana kwenye ngao ya hisani.

Yanga walionekana kuwa na makali zaidi katika dakika za mwanzo na dakika ya tano, mshambuliaji Peter Shalulile aliifungia Yanga bao la kuongoza baada ya kutumia nafasi iliyotengenezwa na kiungo Maxi Nzengeli. Bao hilo liliwapa Yanga matumaini ya kuendeleza ubabe wao dhidi ya Simba, na hadi mapumziko walikuwa mbele kwa bao 1-0 huku Simba ikiongoza kwenye kutawala mchezo huo.

Kipindi cha pili kilianza kwa Simba kuongeza kasi ya mashambulizi wakisaka bao la kusawazisha na jitihada zao zilizaa matunda dakika ya 68, pale kiungo, Neo Maema alipoifungia Simba bao la kusawazisha na kuamsha shangwe kwa mashabiki wa timu hiyo .

Simba waliendelea kuwasakama wapinzani wao na dakika ya 71 Elie Mpanzu alifunga bao la pili lililoipa timu yake ushindi wa mabao 2-1.



Mpanzu alifanya vizuri na kuchaguliwa kuwa mchezaji bora wa mchezo huo kutokana na kiwango kizuri kwenye mchezo huo.

Ushindi huo ulikuwa muhimu kwa Simba katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2026/2027 ambapo kabla ya mchezo huo, timu zote mbili zilikuwa zimekusanya alama 18 baada ya kushinda mechi zao sita za mwanzo.

Matokeo hayo yaliifanya Simba kufikisha alama 21 na kuongoza ligi kwa tofauti ya alama tatu dhidi ya Yanga, ambao walipata kipigo chao cha kwanza katika ligi msimu huu hivyo Simba kubaki timu pekee ambayo haijafungwa msimu huu.

Dabi ya Kariakoo ukiwa ni mchezo wa kukumbukwa kutokana na ushindani mkubwa na uwezo wa Simba kurejea mchezoni baada ya kuruhusu bao la mapema. Ushindi huo umeongeza morali kwa wachezaji na mashabiki wa Simba, huku Yanga wakilazimika kujipanga upya kwa michezo inayofuata.

Pamoja na ushindani huo, mashabiki wa timu zote wanapaswa kuendeleza upendo wa soka, kuheshimiana na kudumisha amani, kwani thamani ya dabi ya Kariakoo haipo katika ushindi pekee, bali pia katika burudani na mchango wake kwa maendeleo ya soka la Tanzania.

FVS: TEKNOLOJIA ILIYOLETA MAGEUZI YA SOKA TANZANIA



Mpira wa miguu ni mchezo unaojengwa kwa ushindani, hisia, mikakati na maamuzi yanayoweza kubadili matokeo ndani ya sekunde chache. Katika mazingira hayo, usahihi wa maamuzi umekuwa moja ya mambo muhimu yanayochangia ubora na uaminifu wa mashindano. Hata hivyo, kwa muda mrefu, baadhi ya matukio yenye utata yamekuwa yakizua mijadala mikubwa, huku makosa ya kibinadamu yakitajwa kuwa sehemu ya changamoto za mchezo huo.

Ligi Kuu ya NBC imeingia katika ukurasa mpya wa maendeleo kupitia matumizi ya teknolojia ya Football Video Support (FVS), mfumo ambao umeanza kuleta mabadiliko katika namna matukio muhimu yanavyopitiwa na kuamuliwa.

Tanzania imekuwa nchi ya kwanza barani Afrika kutumia teknolojia hiyo katika ligi yake ya juu, hatua inayoiweka Ligi Kuu ya NBC katika nafasi muhimu ya kuonyesha namna teknolojia inavyoweza kusaidia maendeleo ya soka la ndani na kimataifa.

FVS si teknolojia inayolenga kuondoa mamlaka ya mwamuzi, bali ni mfumo unaompa nafasi ya kutathmini upya tukio muhimu ambalo huenda hakuliona vizuri wakati mchezo ukiendelea.
Kupitia mfumo huo, makocha wana nafasi ya kuomba mapitio ya matukio maalumu yanayoweza kuathiri matokeo ya mchezo. Mwamuzi huangalia picha za marudio na kubaki na mamlaka ya mwisho ya kufanya uamuzi.

Hii ina maana kwamba soka la Tanzania limeanza kuingia katika mfumo ambao maamuzi muhimu yanaweza kutathminiwa kwa ushahidi wa picha, badala ya kutegemea mtazamo wa awali pekee hivyo kwa ligi yenye ushindani mkubwa kama ya NBC ambapo tofauti ya bao moja inaweza kuamua hatima ya timu, teknolojia hii imekuwa nyenzo muhimu katika kuongeza usahihi wa maamuzi.

Miongoni mwa hatua muhimu zaidi katika safari ya FVS ni matumizi yake katika Kariakoo ‘Derby’ kati ya Simba na Young Africans, mchezo ambao umekuwa na nafasi kubwa katika historia ya soka la Tanzania.

Dabi hiyo ya Oktoba 10, 2026, iliyochezwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, ilikuwa mchezo wa kwanza wa ‘wababe’ hao wa soka la Tanzania wa Ligi Kuu ya NBC kuchezwa na teknolojia ya FVS kutumika.
Kwa mwezi Oktoba FVS imetumika kuamua baadhi ya matukio muhimu ambayo yangeweza kuathiri mchezo, kwa mfano; katika mchezo kati ya TRA na Young Africans teknolojia hiyo ilitumika kuamua kadi nyekundu ya mchezaji wa Young Africans, Mudathir Yahya.
Mchezo mwingine wa mwezi Oktoba uliopata usaidizi wa FVS ni kati ya Fountain Gate na Simba ambapo mwamuzi msaidizi aliona mchezaji wa Simba amefunga bao akiwa kwenye nafasi ya kuotea lakini baada ya kutumia teknolojia hiyo aligundua kuwa lilikuwa bao halali.

Mchezo kati ya Pamba Jiji na Singida Black Stars pia ulishuhudia mwamuzi akifuta maamuzi ya mkwaju wa penati baada ya kujiridhisha kwamba haikua penati halali na pia mchezo kati ya Coastal Union na Azam ulishuhudia zaidi ya bao moja likifutwa kutokana na mchezaji kuwa nafasi ambayo siyo sahihi na endapo teknolojia hii isingekuwepo basi mabao hayo huenda yangesalia.

Hii inaonyesha kuwa teknolojia hii imeleta mageuzi makubwa na kuwa msaada mkubwa sana kwa maendeleo ya soka letu kwani imefanya maamuzi yanayotolewa uwanjani kuwa ya uhakika na yasiyopendelea upande wowote.

FVS haiwezi kuondoa kabisa mijadala ya soka, lakini inaweza kusaidia kupunguza baadhi ya makosa katika matukio muhimu na kuongeza uwazi katika mchakato wa maamuzi.

TPLB YAINGIZA TEKNOLOJIA MPYA LIGI KUU YA NBC

Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) imeongeza hatua mpya za kiusalama katika Ligi Kuu ya NBC kwa kuanzisha matumizi ya kifaa maalumu cha kupima gesi na viwango vya oksijeni ndani ya vyumba vya kubadilishia nguo, hatua inayolenga kuimarisha usalama na ustawi wa wachezaji, makocha pamoja na viongozi wa timu.

Hatua hiyo inaashiria namna ambavyo Bodi ya Ligi inavyoendelea kuboresha usimamizi wa mashindano kwa kutumia teknolojia katika kukabiliana na changamoto zilizokuwa zikijitokeza kwenye baadhi ya viwanja nchini.

Kifaa hicho, kinachojulikana kama ‘Gas Detector’ , kilitangazwa na Mtendaji Mkuu wa TPLB, Cornel Barnabas, kuelekea mchezo wa Kariakoo ‘Derby’ kati ya Simba na Young Africans, uliochezwa Oktoba 10, 2026, katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Suala la mazingira na usalama wa vyumba vya kubadilishia nguo limekuwa miongoni mwa changamoto zinazojadiliwa katika soka la Tanzania, huku baadhi ya klabu zikieleza kutoridhishwa na hali ya vyumba hivyo katika viwanja mbalimbali.

Kupitia kifaa hicho kipya, TPLB inalenga kuimarisha ukaguzi wa mazingira ya vyumba kabla ya wachezaji na viongozi kuvitumia, ili kuhakikisha vinakuwa katika hali inayokidhi viwango vinavyohitajika kwa shughuli za michezo.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Bodi ya Ligi, kifaa hicho kina uwezo wa kupima kiwango cha oksijeni na kubaini uwepo wa gesi zisizofaa katika mazingira husika, huku kikitoa tahadhari pale kinapobaini hali inayohitaji uchunguzi zaidi.

Vyumba vya kubadilishia nguo ni sehemu muhimu ya maandalizi ya kimwili na kiakili ya wachezaji, hivyo kuhakikisha usalama wa mazingira hayo ni hatua inayoweza kuongeza imani ya timu katika miundombinu ya mashindano.

Hata hivyo, matumizi ya vifaa hivyo hayakuishia katika mchezo wa Simba na Yanga pekee, bali yameendelea katika michezo mingine ya Ligi Kuu ya NBC hadi sasa.

Hatua hiyo inaonesha kuwa TPLB inalenga kuifanya teknolojia kuwa sehemu ya kawaida ya usimamizi wa mashindano, badala ya kuitumia katika michezo mikubwa pekee.

Katika kipindi ambacho soka la Tanzania linaendelea kukua na kuvutia wadau wengi zaidi, uwekezaji katika usalama, teknolojia na ubora wa miundombinu ni sehemu muhimu ya maendeleo ya mchezo huo.

Matumizi ya ‘Gas Detector’ yanaweza kuwa mwanzo wa mfumo mpana zaidi wa ukaguzi wa mazingira ya viwanja, ikiwa ni pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya Bodi ya Ligi, wamiliki wa viwanja na klabu zinazoshiriki mashindano.

Teknolojia hiyo mpya inaweka msingi wa usimamizi unaozingatia tahadhari, uwajibikaji na viwango vya kisasa, huku ikiongeza matumaini ya kuona changamoto za kiusalama zikitatuliwa kwa njia za kitaalamu zaidi.





Timu hiyo imefunga mabao 23, ikiwa imeruhusu mabao sita huku na kuwa timu pekee yenye ushindi kwa asilimia 100 hadi sasa kwenye Ligi Kuu ya NBC. Simba inashikilia rekodi ya kushinda mabao mengi kwenye mchezo mmoja baada ya kuifunga Mashujaa mabao 6-1 sawa na Geita Gold iliyoshinda 6-2 dhidi ya Kagera Sugar.

SIMBA SC YATAWALA MSIMAMO WA NBC PREMIER LEAGUE 2026/27

POS	TEAM	P	W	D	L	GF	GA	GD	PTS
1	Simba SC	10	10	0	0	23	6	17	30
2	Young Africans SC	10	8	1	1	23	5	18	25
3	Azam FC	10	7	2	1	19	8	11	23
4	JKT Tanzania	11	5	2	4	13	14	-1	17
5	Dodoma Jiji	10	4	4	2	8	5	3	16
6	Polisi Tanzania	11	4	3	4	13	12	1	15
7	Namungo FC	11	5	0	6	12	15	-3	15
8	Mashujaa FC	10	5	0	5	11	15	-4	15
9	Singida Black Stars	10	4	2	4	15	12	3	14
10	Coastal Union	11	4	2	5	9	13	-4	14
11	Mbeya City	10	4	1	5	9	13	-4	13
12	TRA United SC	10	2	5	3	10	10	0	11
13	Geita Gold	11	2	3	6	11	18	-7	9
14	Pamba Jiji FC	11	1	3	7	10	17	-7	6
15	Fountain Gate	11	1	3	7	7	17	-10	6
16	Kagera Sugar	11	1	3	7	9	22	-13	6

Timu ya Simba inaendelea kutawala msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara msimu wa 2026/27, ikiwa kileleni mwa msimamo kwa alama 30 baada ya kucheza mechi 10 na kushinda zote.

Simba ipo kwenye kiwango bora msimu huu ikilitafuta taji la Ligi Kuu ya NBC ambalo haijafanikiwa kulipata tangu ligi hiyo ianze kutambulika kama Ligi Kuu ya NBC.

Nafasi ya pili inashikiliwa na timu ya Young Africans, yenye alama 25 baada ya kucheza mechi 10, ikishinda nane, kutoka sare moja na kupoteza moja, Young Africans imefunga mabao 23 na kuruhusu matano. Timu ya Azam inashika nafasi ya tatu ikiwa na alama 23 baada ya kucheza michezo 10, ikipata ushindi mara saba, sare mbili na kupoteza mchezo mmoja. Timu hiyo imefunga mabao 19 na kuruhusu mabao nane.

JKT Tanzania inashika nafasi ya nne ikiwa na alama 17 baada ya kucheza michezo 11, ikiwa ni ushindi mara tano, sare mbili na kupoteza michezo minne, timu hiyo imefunga mabao 13 na kuruhusu mabao 14 ndani ya msimu huu wa Ligi Kuu ya NBC. Nafasi ya tano inashikiliwa na timu ya Dodoma Jiji yenye alama 16 baada ya kucheza mechi 10, ikishinda nne, kupata sare nne na kupoteza michezo miwili, huku timu hiyo ikifanikiwa kupata mabao nane na kuruhusu mabao matano.

Polisi Tanzania inashika nafasi ya sita na alama 15, sawa na Namungo iliyo nafasi ya saba na Mashujaa iliyo nafasi ya nane. Polisi Tanzania imecheza mechi 11 ushindi nne sare tatu na kufungwa nne huku Namungo yenye michezo 11 ushindi tano na kufungwa sita. Mashujaa ikiwa imecheza mechi 10 sawa na ushindi tano na kufungwa michezo mitano.

Singida Black Stars inashika nafasi ya tisa kwa kukusanya alama 14 baada ya kucheza mechi tisa, ikiwa na ushindi mara nne, sare mbili na kupoteza mara tatu ndani ya msimu wa 2026/2027 wa Ligi Kuu ya NBC, aidha imefunga mabao 15 na kuruhusu 11.

Coastal Union ipo nafasi ya 10 baada ya kucheza michezo 11 kushinda michezo minne sare mbili na kufungwa michezo miwili huku ikivuna alama 14 baada ya kufunga mabao tisa na kuruhusu 13.

TRA United inashika nafasi ya 11 kwa kuvuna alama 11 baada ya kucheza michezo 10, ushindi michezo miwili, sare tano na kufungwa michezo mitatu aidha imefunga mabao 10 na kufungwa mabao 10.

Mbeya City inashika nafasi ya 12 ikiwa na alama 10, sawa na michezo tisa ambapo timu hiyo imeshinda michezo mitatu, sare moja na kufungwa michezo mitano huku ikifunga mabao nane na kufungwa mabao 13.

Geita Gold iliyo nafasi ya 13 imecheza michezo 11 ikiwa na ushindi mara mbili, sare tatu na kupoteza michezo sita huku ikiungana na Simba kuwa timu iliyofunga mabao mengi kwenye mchezo mmoja baada ya kuifunga Kagera Sugar mabao 6-2 kwenye uwanja wa Bukombe, Geita.

Katika nafasi ya 14 ipo Pamba Jiji ikiwa na alama sita baada ya kucheza mechi 11, ikiwa na ushindi mmoja, sare tatu na kupoteza michezo saba, aidha timu hiyo imefunga mabao 10 na kuruhusu mabao 17.

Fountain Gate inashika nafasi ya 15, ikiwa na alama sita baada ya kucheza mechi 11. Timu hiyo imeshinda mchezo mmoja, sare tatu na kupoteza michezo saba huku ikiwa imefunga mabao saba na kuruhusu 17.

Kagera Sugar ipo nafasi ya 16 baada ya kucheza michezo 11 ikiwa ushindi ni mmoja sare tatu na kufungwa michezo saba, aidha imeweza kuvuna alama sita huku ikifunga mabao tis ana kufungwa 22.





SIRI NYUMA YA ‘UNBEATEN’ ZA SIMBA, AZAM, DODOMA JIJI LIGI KUU YA NBC.

Na **Sisti Martin** sistinho

MWEZI Oktoba 2026 umekuwa na ushindani mkubwa katika Ligi kuu ya NBC, huku timu kadhaa zikikabiliwa na changamoto ya kudumisha matokeo chanya katika ratiba ya michezo ya ligi hiyo.
Hata hivyo timu za Simba, Azam na Dodoma Jiji zimeweza kumaliza mwezi huo bila kupoteza mchezo wowote wa ligi, jambo linaloonesha viwango tofauti vya mwendelezo wa matokeo mazuri katika ushindani wa ligi hiyo.

Ingawa timu zote tatu zimefanikiwa kuepuka kipigo, namna zilivyofikia mafanikio hayo inatofautiana. Simba na Azam zimeonesha uwezo mkubwa wa kubadilisha ubora wa mchezo kuwa ushindi, wakati Dodoma Jiji imeonesha umuhimu wa uzuiaji bora na uwezo wa kupata matokeo katika michezo yenye ushindani mkubwa.

Simba imekuwa miongoni mwa timu zilizofanya vizuri zaidi katika mwezi Oktoba. Katika michezo mitatu iliyokamilika ndani ya mwezi huo, Simba ilipata ushindi dhidi ya Young Africans (2-1), Mashujaa (6-1) na Fountain Gate (1-0), ikikusanya alama tisa kati ya tisa zilizokuwa kwenye ushindani kiasi cha kocha wake Steve Barker kuweza kuwa kocha bora wa mwezi.

Silaha kubwa ya Simba ni kufunga idadi kubwa ya mabao zaidi ya wapinzani kwani kwenye mechi zao mbili kati ya tatu imeruhusu kufungwa bao, ambapo kwenye mchezo dhidi ya Young Africans na Mashujaa iliruhusu kufungwa bao kwenye kila mchezo huku wakiruhusu kwenye nyakati ngumu mfano bao la shuti la mbali dhidi ya Mashujaa lililofungwa na Seleman Bwenzi na bao la shambulizi la kujibu walilofungwa dhidi ya Young Africans punde tu baada ya kupoteza umiliki wa mpira (Offensive Transition), bao walilofungwa na Peter Shalulile baada ya Max Nzengeli kupora mpira. Kwenye ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya Mashujaa, ushindi wa 2-1 dhidi ya Young Africans na ushindi wa 1-0 dhidi ya Fountain Gate, ulishuhudia mabao kutoka kwenye nyakati tofauti ambapo mabao manne walifunga timu yao ikiwa na mpira kwa kujenga shambulizi na kupenya kuta za uzuiaji za wapinzani wao (In Possession Moments), mabao matatu wakifunga kwa mipira ya kutenga kama pigo huru dhidi ya Fountain na dhidi ya Mashujaa FC (Set Plays).

Kwa tathmini, Ubora wa Simba ulikuwa kwenye nyakati zao za kushambulia kuweza kutengeneza nafasi nyingi za kufunga licha ya kuruhusu kufungwa mabao mawili kwenye mechi hizo tatu huku mchezaji wao Elie Mpanzu akiweza kuibuka mchezaji bora wa mwezi kwa kufunga mabao matatu kwenye mechi tatu.

Azam FC nayo imeonyesha kiwango kizuri katika mwezi Oktoba, ikimaliza michezo yake mitatu ya ligi bila kupoteza. Ushindi dhidi ya Coastal Union (2-0), Mbeya City (4-0) na JKT Tanzania (2-1) uliifanya timu hiyo kukusanya alama tisa.



Kitu kinachovutia katika mwenendo wa Azam ni uwezo wake wa kuzalisha mabao katika mazingira tofauti ya ushindani. Ushindi wa 2-0 dhidi ya Coastal Union ulionesha uwezo wa kupata matokeo ugenini, wakati ushindi wa 4-0 dhidi ya Mbeya City uliipa timu nafasi ya kuonesha ubora wake katika eneo la ushambuliaji.

Utawala wa mchezo wa Azam ulianzia kwenye nyakati ambazo timu yao ilikuwa na umiliki wa mpira (In Possession Moments) ambapo ilitawala vizuri umiliki wa mpira na kutengeneza nafasi za kufunga ambapo kwenye nyakati hizo imefanikiwa kufunga mabao matano mfano ni mabao mawili dhidi ya Coastal Union yaliyofungwa na Enock Molia na Feisal Salum.

Pia Azam iliweza kutawala nyakati ambazo timu yao haikuwa na umiliki wa mpira (Out of Possession) ambapo imefanikiwa kupata hati safi kwenye mechi mbili kati ya tatu, ikikosa hati safi kwenye mchezo dhidi ya JKT Tanzania pekee ambapo waliruhusu kufungwa bao lililofungwa na Karim Mfaume.

Azam haikuwa nyuma kutumia vizuri mipira ya kutenga ambapo kati ya mabao nane waliyofunga, mabao mawili yametokana na mipira ya kutenga (Set Plays) na yote ni dhidi ya JKT Tanzania yaliyotokana na Pigo huru (Free-kick) lililofungwa na Iddi Seleman ‘Nado’ na kona iliyofungwa na Lusajo Mwaikenda.

Tofauti na Simba na Azam, Dodoma Jiji imefikia mwisho wa Oktoba ikiwa na ushindi mmoja na sare tatu katika michezo minne, lakini jambo muhimu ni kwamba haikupoteza mchezo wowote.





Dodoma Jiji ilianza kwa sare ya 1-1 dhidi ya Singida Black Stars, ikafuatiwa na ushindi wa 3-0 dhidi ya Geita Gold. Baadaye ilitoka sare tasa ya 0-0 dhidi ya JKT Tanzania na Coastal Union.

Katika michezo hiyo minne, Dodoma Jiji ilifunga mabao manne na kuruhusu bao moja pekee, huku ikikusanya alama sita kati ya 12 zilizokuwa kwenye ushindani.

Takwimu hii inaweka wazi jambo moja muhimu: mafanikio ya Dodoma Jiji katika Oktoba yalijengwa zaidi na uwezo wa kiuzuiaji kuepuka vipigo na kudhibiti hatari ya kuruhusu mabao mengi ambapo kipa wao Musa Mbissa alifanikiwa kupata hati safi tatu huku akiokoa mashuti 'saves' sita kwenye mechi hizo minne.

Kuruhusu bao moja pekee katika michezo minne ni kiashiria kizuri cha matokeo ya uzuiaji bora ambao pia uliweza kuzalisha mabao kwao kwani uzuiaji wao bora uliwafanikisha kuweza kupora mipira na kufanya mashambulizi ya kujibu, mfano ni magoli mawili ya Khelfin Hamdoun dhidi ya Geita Gold.

Wakiwa na umiliki wa mpira Dodoma Jiji ilikuwa timu inayopenda kushambulia kwa mashambulizi ya moja kwa moja ya haraka mfano ni aina ya bao walilofunga dhidi ya Geita Gold ambapo mpira wa pasi ndefu ulitoka kwa kipa Musa Mbissa hadi kwa mshambuliaji Faraji Kayanda aliyepika goli kwa Mwana Kibuta.

Dodoma Jiji ilitumia vizuri nafasi ya mipira ya kutenga kwani kati ya mabao yao manne waliyofunga, bao moja wamepata kupitia mpira wa kutenga, bao la kona dhidi ya Singida BS lililofungwa na Andy Bikoko.

Kumaliza mwezi bila kupoteza ni mafanikio muhimu, lakini katika soka, matokeo yanapaswa kuwa na mwendelezo bora, Simba imeonesha ubora katika kukusanya alama zote zilizokuwa kwenye michezo yake, Azam imeonesha uwiano mzuri wa uzalishaji wa mabao na ulinzi, wakati Dodoma Jiji imeonesha umuhimu wa uzuiaji bora katika kupata matokeo.

Hata hivyo, changamoto ya timu hizi katika miezi inayofuata itakuwa kudumisha mwendelezo wa kiwango hicho. Katika ligi yenye ushindani mkubwa, mafanikio ya muda mfupi yanahitaji kuungwa mkono na ubora wa kiufundi na uwezo wa kufanya maamuzi sahihi katika nafasi zote za mchezo.

LIGI KUU YA NBC NA REKODI MFULULIZO MASHINDANO YA KIMATAIFA

TIMU nne zinazoshiriki Ligi Kuu ya NBC msimu wa 2026/2027 zimefuzu hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Mabingwa Afrika (CAF Champions League) na michuano ya Kombe la Shirikisho (Caf Confederation Cup) ikiwa ni mara ya pili mfululizo timu zote nne kufuzu hatua hiyo.

Timu hizo ni Young Africans na Simba zilizofuzu Ligi ya Mabingwa msimu wa 2026/2027 huku timu za Azam na Singida Black Stars zikifuzu michuano ya Kombe la Shirikisho.

Ligi Kuu ya NBC kwa mujibu wa International Federation of Football History and Statistics (IFFHS) ni Ligi ya sita kwa ubora barani Afrika huku ikishika nafasi ya 54 duniani.

Msimu wa 2026/2027, Ligi Kuu ya NBC imepata mafanikio makubwa baada washiriki wake wote kufuzu na kuingia hatua ya makundi huku Young Africans ikiweka rekodi ya kufuzu kwa mara ya nne mfululizo na timu ya Simba ikiweka rekodi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa mara saba.


Young Africans imevuka hatua hiyo baada ya hatua ya awali kuzifunga timu za Gaborone United ya Botswana kwa matokeo ya jumla ya 3-2 na CFFA Andoharanofotsy ya Madagascar kwa matokeo ya jumla ya 8-1 matokeo yaliyowapa nafasi ya kuendelea na safari ya kuwania ubingwa wa Afrika katika hatua ya makundi.

Simba imefuzu hatua hiyo baada ya kukutana na Might Wanderers ya Malawi kwenye hatua ya awali na kupata matokeo ya jumla ya 7-1 kisha kukutana na 15 de Agosto ya Equatorial Guinea katika mchezo wake wa pili na kuondoka na ushindi wa jumla ya mabao 9-1, hivyo kujihakikishia nafasi ya kuendelea na mashindano hayo kwa hatua ya makundi.

Timu ya Azam imekata tiketi yake hatua ya makundi baada ya kuiondoa Zed ya Misri kwa jumla ya mabao 2-1, ambapo katika mchezo wa kwanza uliochezwa Cairo timu hizo zilitoka sare ya 1-1 kabla ya Azam kutumia vizuri mchezo wa marudiano nyumbani katika uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam na kushinda bao 1-0 hivyo kufuzu hatua ya makundi.

Kwa upande wa Singida Black Stars ilicheza mchezo wa kwanza wa hatua ya awali na timu ya Al-Ghazal na kuifungisha 'virago' kwa jumla ya 10-1 kisha kukutana na Tusker ya Kenya na kuiondoa kwa jumla ya mabao 2-1, Singida ilianza kwa ushindi wa bao 1-0 katika mchezo wa ugenini jijini Nairobi na baada ya kukutana tena katika mchezo wa marudiano ndani ya Azam Complex Dar es Salaam, mchezo ulimalizika kwa sare ya 1-1 na kuitengenezea nafasi nzuri timu ya Singida Black Stars kuendelea na hatua ya makundi ndani ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF Confederation Cup).

Kwa ujumla, uwepo wa klabu nne za Young Africans, Simba SC, Azam Pamoja na Singida Black Stars katika mashindano ya CAF msimu wa 2026/2027 unaongeza matumaini kwa mashabiki na wadau wa soka nchini na namna ambavyo soka la Tanzania linazidi kukua kwa kasi kubwa.



Issa Abushiri

‘BOLI’ & ‘FASHENI’

Steven Barker







NBC CHAMPIONSHIP 'NGOMA INOGILE'

LIGI ya Championship ya NBC imeendelea kushika kasi kwenye viwanja mbali mbali huku timu ya KMC ikiwa timu pekee ambayo haijapoteza mchezo wowote hadi sasa.

KMC ya Dar es Salaam ni kinara wa Ligi ya Championship ya NBC ikiwa imeshinda michezo mitano na sare michezo mitatu, ikifunga jumla ya mabao 16 na kuruhusu mabao matano.

Tanzania Prisons ya Mbeya inashika nafasi ya pili ikiwa imecheza michezo nane na kukusanya alama 16, imeshinda michezo mitano sare moja na kupoteza michezo miwili, pia imefunga mabao 13 na kuruhusu mabao matano.

Mtibwa Sugar ya Morogoro inashika nafasi ya tatu ikiwa imecheza michezo nane na kuvuna alama 15, imeshinda michezo minne sare tatu na kupoteza michezo mmoja huku ikifunga mabao tisa na kuruhusu mabao sita.

Bandari Tanzania ya Mtwara ambayo ni moja ya timu zilizopanda daraja kutoka First League inashika nafasi ya nne kwenye msimamo ikiwa imecheza michezo nane na kukusanya jumla ya alama 14, ikishinda michezo minne sare mbili na kupoteza michezo miwili huku ikiwa imefunga mabao 11 na kuruhusu mabao matano.

Rhino Rangers ya Tabora iliyopanda daraja pia kutoka First League inashika nafasi ya tano ikiwa imecheza michezo nane na kuvuna alama 14, pia timu hiyo imeshinda michezo minne sare mbili na kupoteza michezo miwili huku ikiwa imefunga mabao sita na kuruhusu mabao matatu.

Transit Camp ya Dar es Salaam inashika nafasi ya sita ikiwa na alama 13, imecheza michezo nane kushinda michezo minne sare moja na kupoteza michezo mitatu pia imefunga jumla ya mabao 11 na kuruhusu mabao kumi.

Stand United ya Shinyanga ipo nafasi ya saba ikiwa na alama 13 baada ya kucheza michezo nane na kushinda michezo minne sare moja na kupoteza michezo mitatu, aidha imefunga jumla ya mabao 10 na kuruhusu mabao tisa.

Kigamboni United ya Dar es Salaam inashika nafasi ya nane ikiwa na alama 12 baada ya kucheza michezo nane sawa na kushinda michezo mitatu, sare tatu na kufungwa michezo miwili huku pia imefunga jumla ya mabao tisa na kuruhusu mabao saba.

IAA ya Arusha iliyotoka First League baada ya kuifunga African Sports kwenye mchezo wa hatua ya mtoano inashika nafasi ya tisa ikiwa na alama 10 baada ya kucheza michezo nane na kushinda michezo miwili, sare nne na kupoteza michezo miwili huku pia ikifunga mabao nane na kuruhusu mabao 10.

Gunners ya Dodoma inashika nafasi ya 10 ikiwa imecheza michezo saba na kukusanya alama nane kwa kushinda mchezo mmoja sare tano na kupoteza michezo miwili huku ikiwa imefunga mabao sita na kuruhusu mabao saba.

Kengold inashika nafasi ya 11 ikiwa imecheza michezo nane na kuvuna alama nane huku ikiwa imeshinda michezo miwili, sare miwili na kupoteza michezo mine, imefunga mabao 10 na kuruhusu mabao 13.

Mbuni inashika nafasi ya 12 ikiwa imecheza michezo nane na kukusanya alama tano huku ikiwa imeshinda michezo miwili sare mbili na kupoteza michezo mine, imefunga mabao tisa na kuruhusu mabao 14.

Tabora United inashika nafasi ya 13 ikiwa na alama saba baada ya kucheza michezo nane na kupata ushindi mara mbili, sare moja na kupoteza michezo mitano, imefunga mabao 10 na kuruhusu mabao 14.

Bigman inashika nafasi ya 14 baada ya kucheza michezo nane na kuvuna alama saba, ikiwa imeshinda michezo miwili sare moja na kupoteza michezo mitano huku ikiwa imefunga mabao 10 na kuruhusu mabao 16.

Songea United inashika nafasi ya 15 ikiwa imecheza michezo nane na kuvuna alama sita ushindi mchezo mmoja, kupoteza michezo minne na sare tatu huku ikiwa imefunga mabao manne na kuruhusu mabao tisa.

TMA inashika nafasi ya 16 ikiwa imecheza michezo nane na kukusanya alama mbili baada kushinda mchezo mmoja, sare michezo miwili na kupoteza michezo miwili huku ikifunga mabao matatu na kuruhusu mabao 14. Timu hiyo ilipoteza mchezo mmoja kwa mabao 3-0 kama adhabu ya kushindwa kufika uwanjani dhidi ya Stand United huku pia ikipokwa alama tatu.



PAZIA LA FIRST LEAGUE 2026/27 LAFUNGULIWA.

LIGI ya First League msimu wa 2026/27 imeanza rasmi Oktoba 29, 2026, ikifungua ukurasa mpya wa ushindani katika mbio za kuwania mafanikio na nafasi za kupanda daraja. Michezo ya ufunguzi katika Kundi A na Kundi B imeshuhudia ushindi wa mabao na matokeo huku baadhi ya timu zikianza safari yao kwa kupata alama tatu muhimu.

Katika Kundi A, Cosmopolitan ilianza kampeni yake kwa kishindo baada ya kuichapa Pan African mabao 3-0, matokeo yaliyoiweka katika nafasi nzuri ya kuanza safari ya kuwania mafanikio msimu huu. Nyumbu nayo ilionyesha uwezo wa kushambulia baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Magnet, katika mchezo uliokuwa na ushindani mkubwa.

Hausang pia ilianza msimu kwa mafanikio baada ya kuifunga Barberian bao 1-0, ikipata ushindi mwembamba lakini muhimu katika mchezo wake wa kwanza. Kwa upande mwingine, Dar City na Moro Kids zilishindwa kutofautiana baada ya kutoka suluhu kwenye matokeo yaliyoifanya kila timu kuondoka na alama moja katika mchezo huo.

Kundi B lilishuhudia michezo yenye ushindani na mabao mengi zaidi. Madini FC ilikuwa miongoni mwa timu zilizotoa burudani katika siku ya ufunguzi baada ya kuichapa Alliance mabao 4-2, katika mchezo uliokuwa na jumla ya mabao sita. Ushindi huo unaipa Madini mwanzo mzuri katika harakati zake za kuwania mafanikio ya msimu.

Kigoma FC nayo ilianza kwa ushindi baada ya kuifunga Hanang bao 1-0, huku NKIM ikipata alama tatu muhimu kwa kuichapa African Sport mabao 2-1. Katika mchezo mwingine wa kundi hilo, Copco na Endument zilitoshana nguvu kwa kutoka sare ya mabao 2-2, zikigawana alama katika mchezo uliokuwa na ushindani.

Kwa ujumla, michezo ya ufunguzi wa Ligi ya First League imeonesha ushindani mkubwa katika makundi yote mawili, huku timu zikianza kuweka msingi wa safari yao ya msimu. Ushindi wa Cosmopolitan, Nyumbu, Hausang, Madini, Kigoma na NKIM umeweka mazingira ya ushindani mapema, lakini sare za Dar City dhidi ya Moro Kids na Copco dhidi ya Endument zinaonesha kuwa kila alama itakuwa na umuhimu katika mbio za msimu huu.

Kadri ligi inavyoendelea, macho ya mashabiki yataelekezwa katika namna timu zitakavyodumisha viwango vyao, kujipanga kwa michezo inayofuata na kuendelea kupambana katika safari ya kuwania mafanikio ya msimu huu.



TUNAKUONA MBALI

DIASPORA

NBC

Benki ya Taifa ya Biashara

Daima Karibu Nawe.

Usiache ndoto zako ziishie mbali

Pandisha mjengo wako nyumbani bila wasiwasi



Twiga Diaspora Banking

Tucheki

nbc_diasporabanking@nbc.co.tz